WITO WA MAANDIKO YA MIRADI KWA AJILI YA UFADHILI KUTOKA MFUKO WA UHIFADHI WA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund-EAMCEF) KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022

1. Utangulizi

Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund-EAMCEF) ni Mfuko wa Udhamini (Trust Fund) ulioanzishwa kama mkakati mahususi wa muda mrefu na wa uhakika wa kufadhili miradi ya maendeleo ya jamii, uhifadhi wa bioanuwai na tafiti muhimu katika Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania. Miradi hii ni ile inayochangia katika ustawishaji wa bioanuwai, mfumo-ikolojia na matumizi endelevu ya maliasili zilizomo kwenye Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania. Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ulianzishwa kwa jitihada za pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe waanzilishi wa Bodi ya Wadhamini (Founder Trustees), Benki ya Dunia (World Bank-WB) na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility-GEF). EAMCEF ilisajiliwa rasmi nchini Tanzania tarehe 6 Juni 2001 chini ya Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini (Sura ya 318 Toleo la 2002). EAMCEF ni Taasisi huru, inayojitegemea na isiyotengeneza faida iliyoanzishwa mahususi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha wa uhakika na wa muda mrefu ili kuunga mkono jitihada za uhifadhi endelevu wa maliasili zilizomo kwenye Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania. Shughuli za kila siku za EAMCEF hutekelezwa na Sekretarieti ya Mfuko iliyopo Mjini Morogoro chini ya Mkurugenzi Mtendaji na inayosimamiwa na Bodi ya Wadhamini.

Milima ya Tao la Mashariki ina eneo la ardhi lenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 5,350 lililopo katika Wilaya kumi na tano (15) za mikoa mitano (5) nchini Tanzania - Tanga (Milima ya Usambara Magharibi, Usambara Mashariki na Nguu) Wilaya za Lushoto, Korogwe, Muheza, Mkinga na Kilindi; Kilimanjaro (Milima ya Upare Kaskazini na Upare Kusini) Wilaya za Mwanga na Same; Morogoro (Milima ya Nguru, Uluguru, Ukaguru, Udzungwa, Malundwe, Mahenge na Rubeho) Wilaya za Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kilombero, Ulanga na Manispaa ya Morogoro; Dodoma (Milima ya Rubeho) Wilaya ya Mpwapwa na Iringa (Milima ya Udzungwa) Wilaya za Mufindi na Kilolo.

2. Maeneo lengwa

Mnamo mwaka 2006 EAMCEF ilianza kufadhili miradi ikilenga Hifadhi nne za Misitu ya Mazingira Asilia (Nature Forest Reserves) za Amani (Amani Nature Forest Reserve) wilayani Muheza na Korogwe; Nilo (Nilo Nature Forest Reserve) wilayani Muheza, Korogwe na Mkinga; Kilombero (Kilombero Nature Forest Reserve) wilayani Kilolo na Kilombero na Uzungwa Scarp (Uzungwa Scarp Nature Forest Reserve) wilayani Kilolo, Mufindi na Kilombero. Kuanzia mwezi June 2011 EAMCEF ilipanua ufadhili wake katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia zingine tano (5) - Uluguru (Uluguru Nature Forest Reserve) wilayani Mvomero, Morogoro na Manispaa ya Morogoro; Mkingu (Mkingu Nature Forest Reserve) wilayani Mvomero; Magamba (Magamba Nature Forest Reserve) wilayani Lushoto na Korogwe; Chome (Chome Nature Forest Reserve) wilayani Same na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa (Udzungwa Mountains National Park) wilayani Kilombero na Kilolo kufuatia hisani ya ufadhili wa Serikali ya Ufalme wa Norway

na hivyo kufanya idadi ya Hifadhi zinazofadhiliwa na EAMCEF hadi sasa kufikia tisa (9) kwenye Halmashauri za Wilaya kumi na moja (11).

3. Nani Anaweza Kuomba Ufadhili

Maandiko ya miradi yanakaribishwa kutoka katika Idara za Serikali (Serikali Kuu na Serikali za Mitaa), Asasi za Kiraia, Asasi za Kijamii, Wananchi Kutoka kwenye Maeneo Lengwa, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu ya Juu, Makampuni na Watu Binafsi wenye nia ya kufanya kazi katika maeneo husika. Maandiko yenye kukidhi vigezo yatakayowasilishwa na taasisi na asasi mbalimbali kutoka kwenye wilaya lengwa yatapewa kipaumbele katika ufadhili wa EAMCEF.

4. Aina Kuu za Miradi

- Shughuli za maendeleo ya jamii zinazochangia katika uhifadhi wa bioanuwai na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza umasikini na kuboresha ustawi wa maisha ya jamii zinazopakana na misitu ya Milima ya Tao la Mashariki,
- Shughuli za utafiti unaolenga kuboresha uhifadhi wa bioanuwai na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo lengwa ya Milima ya Tao la Mashariki,
- Shughuli za utunzaji na usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuimarisha mifumo-ikolojia ya Milima ya Tao la Mashariki na kuboresha uwezo wa usimamizi wa taasisi husika.

5. Vigezo vya Ufadhili wa Miradi

Miradi inayofadhiliwa na EAMCEF ni ile yenye kuleta tija katika uhifadhi wa bioanuwai na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye misitu lengwa ya Milima ya Tao la Mashariki. Sharti lingine muhimu ni kwamba, ufadhili wa EAMCEF siyo mbadala wa ufadhili kutoka kwa wadau wengine bali unalenga kuchangia katika jitihada za uhifadhi zilizopo kwenye maeneo husika.

Vigezo vingine ni pamoja na:

- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zinawiana na mipango ya usimamizi na vipaumbele vya uhifadhi wa misitu husika;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia kuimarisha usimamizi wa rasilimali zilizomo kwenye misitu ya maeneo lengwa;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zinaweza pia kutekelezwa katika maeneo lengwa mengine au kwenye Milima ya Tao la Mashariki kwa ujumla;
- Uchangiaji wa matokeo chanya ya uhifadhi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki (kwa mfano kupunguza matumizi ya rasilimali zilizomo kwenye misitu husika);
- Utambuzi wa shughuli za awali na zinazoendelea katika eneo lengwa pamoja na uwiano na uhusiano wake;
- Ushiriki wa jamii husika (kwa mfano uwakilishi, kiwango cha ushiriki wa jamii katika kubaini shughuli za mradi, uendelezaji na utekelezaji wake);
- Uzingatiaji wa masuala ya mazingira, hususan katika kulinda bioanuwai na rasilimali nyingine muhimu na athari zake kwenye maeneo yaliyohifadhiwa;
- Kiwango ambacho uhifadhi wa mazingira na maliasili zake utachangia katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha jamii husika;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia katika kuzuia na/au kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia katika kubadilisha tabia za jamii za kuharibu mazingira katika maeneo lengwa;

- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia katika kuongeza manufaa kwa bidhaa zitokanazo na miradi iliyofadhiliwa awali na EAMCEF;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia katika kushughulikia changamoto za masoko kwa bidhaa zitokanazo na miradi inayofadhiliwa na EAMCEF;
- Kiwango ambacho shughuli zinazopendekezwa zitachangia katika kuhamasisha maendeleo na ukuzaji wa biashara;

Vigezo vya ziada

(a) Miradi ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi: Miradi ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi ni budi pia izingatie vigezo vifuatavyo:

- Mchango wa mradi katika ushirikishwaji wa jamii kwenye uendelezaji na usimamizi wa misitu ya asili kwenye eneo lengwa;
- Umuhimu na thamani ya uhifadhi wa eneo husika katika ulinzi wa misitu;
- Mchango wa mradi husika katika kushughulikia changamoto za thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zitokanazo na miradi ya kujiongezea kipato;
- Kiwango cha ufanisi na uendelevu wa mradi unaopendekezwa kwa kuzingatia viashiria kama:

    - Usimamizi unaojitosheleza;
    - Urahisi wa utekelezaji;
    - Fursa za masoko;
    - Thamani ya rasilimali fedha;
    - Kiwango cha ushiriki na dhamira ya jamii husika;
    - Kipaumbele cha uhifadhi katika jamii husika
    - Mambo mengine yanayoweza kuathiri utekelezaji wa mradi.
- Kiwango cha athari za kiuchumi na adha kwa jamii zitokanazo na utekelezaji wa sera za misitu katika eneo husika
- Kiwango cha athari kwa jamii zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi
- Kiwango cha utayari wa jamii
- Kiwango cha kiuchumi cha jamii pamoja na uwepo au ukosefu wa fursa ya kupata fedha kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya mradi unaopendekezwa.
- Mambo mengine muhimu yanayoweza kuathiri uhifadhi

Mifano ya Miradi ya Jamii inayoweza kufadhiliwa na EAMCEF ni pamoja na:

- Shughuli za utalii-ikolojia (kama vile: maeneo ya kambi za kitalii, safari za kuangalia ndege, safari za matembezi ya kitalii, shughuli za kitamaduni, sanaa za mikono, huduma za kuongoza watalii, usafirishaji wa watalii, mafunzo kwa waongoza watalii, utafutaji masoko, nyumba za kulala watalii, nk);
- Shughuli za misitu (mfano: kilimo-misitu, mashamba ya miti, uboreshaji wa uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya shoroba za misitu, uendelezaji wa bidhaa zisizo timbao, miongoni mwa mambo mengine);
- Miradi ya elimu kama vile upanuzi wa shule, mifuko ya elimu, ufadhili wa wanafunzi, elimu ya uhifadhi, programu za elimu ya mazingira kwa viongozi wa jadi na wanafunzi wa shule, ziara za mafunzo, uimarishaji wa mawasiliano miongoni mwa jamii, nk;
- Miradi ya afya kama vile mpango wa bima ya afya kwa jamii, kupanua zahanati na vituo vya afya;
- Teknolojia za nishati mbadala kwa mfano majiko banifu ya kuni na mkaa, nishati ya jua, bayogesi, n.k.
- Kuboresha upatikanaji wa maji kama vile visima vifupi, pampu za mkono, kulinda chemichemi na vyanzo vingine vya maji;

- Miradi ya mifugo kama vile majosho, huduma za chanjo, ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, ufugaji wa kuku, ufugaji wa nguruwe;
- Miradi ya uzalishaji mali kama vile masoko ya asali, utengenezaji wa vikapu/mifuko ya asili kwa ajili ya kuuzia watalii, pembejeo za kilimo (kwa mfano viuatilifu kwa ajili ya mbogamboga kama nyanya nk). Vyama vya ushirika vinaweza kuwa na sifa kwa aina hii ya miradi; na,
- Miradi na shughuli za kilimo-misitu zinazozingatia uhifadhi na kilimo ikolojia kama vile matumizi ya samadi, kilimo cha makinga maji/matuta, bustani za nyumbani, kilimo-hifadhi, n. k.;
- Shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama vile shughuli mbadala za kujipatia kipato, vyanzo mbadala vya nishati, n.k.;
- Shughuli na miradi mingine kama vile kuimarisha miundombinu (barabara za vijijini, madaraja, maji, nishati), shughuli za kuongeza kipato na oboreshaji wa ustawi wa maisha ya jamii na vikundi vya kijamii.

(b) Miradi ya Utafiti wa Bioanuwai na Mabadiliko ya Tabianchi itachaguliwa kwa kuzingatia umuhimu wa miradi husika katika uhifadhi wa bioanuwai kwenye Milima ya Tao la Mashariki. Miradi ya tathmini na uperembaji; tathmini ya upungufu wa maarifa, makabiliano na athari za mabadiliko ya tabianchi, upatikanaji endelevu wa rasilimali fedha; utafutaji taarifa msingi kama vile za uvyonzaji wa hewaukaa, kuzuia uchafuzi wa mazingira, kuongeza uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; upembuzi yakinifu, utafiti wa masuala ya kiuchumi na kijamii, tathmini ya thamani ya huduma za kiikolojia (mfano ulipiaji wa huduma za maji, hewa ukaa, bioanuwai n.k.); maeneo yaliyoachwa nyuma kitafiti yatapewa kipaumbele katika ufadhili wa EAMCEF. Vigezo vingine vya miradi ya utafiti ni pamoja na kuonyesha jinsi matokeo ya tafiti husika yatakavyochangia katika kupunguza uharibifu na kuboresha uhifadhi wa maeneo lengwa kwenye Milima ya Tao la Mashariki (kwa mfano kuibua bidhaa mbadala ya matumizi ya rasilimali za misitu, teknolojia rahisi na madhubuti za matumizi ya rasilimali za misitu ya asili). Uwasilishaji na usambazaji wa matokeo ya utafiti ni kigezo cha lazima kwa miradi yote ya utafiti.

(c) Miradi Maalumu kwa ajili ya Uboreshaji wa Maeneo Yaliyohifadhiwa na Ustawi wa Jamii Zinazopakana na Maeneo Husika: EAMCEF itafadhili pia miradi michache itakayojumuisha shughuli za uhifadhi na maendeleo ya jamii katika mfumo-ikolojia mmoja. Miradi hii itafanyika kama majaribio (pilot) na itahusisha wataalamu mbalimbali wenye fani za uhifadhi wa bioanuwai na maendeleo ya jamii. Maandiko ya miradi hii yanapaswa kuonyesha jinsi shughuli pendekezwa zitakavyoweza kuchangia kwenye uhifadhi wa eneo husika na ustawi wa jamii mkabala.

6. Mambo Mengine Muhimu katika Uandaaji wa Maandiko ya Miradi

6.1 Aina ya Ufadhili Uliopo

EAMCEF inatoa aina tatu za ufadhili wa miradi kama sehemu ya programu yake kwa ujumla:

(i) Ufadhili wa Miradi Midogo-Midogo (*Kiwango kisichozidi shilingi milioni 10.0.)*

Mfuko utafadhili miradi midogo-midogo kusaidia jitihada za jamii katika uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki kwenye kila mojawapo ya aina zake kuu tatu za kipaumbele kama zilivyoelezewa hapo juu. Ufadhili wa aina hii unaweza pia kutolewa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na uchambuzi muhimu. Kiwango cha juu kinachoweza kutolewa na EAMCEF kwenye ufadhili huu hakitazidi shilingi milioni 10.0. Kwa kawaida muda wa utekelezaji wa mradi ni kati ya miezi sita na mwaka mmoja.

(ii) Ufadhili wa Miradi ya Kati/Vipindi Maalumu ***(Kiwango kinachozidi shilingi milioni 10.0 hadi shilingi milioni 100.0 kwa mwaka)****.*

Mfuko utafadhili miradi ya vipindi vya kati itakayotekelezwa kwa muda usiozidi miezi thelathini na sita (miaka mitatu) chini ya aina zake kuu tatu za kipaumbele cha ufadhili wake. Kwa ujumla miradi hii haitazidi shilingi milioni 100.0 na mingi yake itakuwa kwenye wastani wa kati ya shilingi milioni ishirini (20) na milioni hamsini (50) kwa mwaka.

(iii) Ufadhili wa Programu na Miradi ya Muda Mrefu (*Kiwango kinachozidi shilingi milioni 10.0 hadi milion 100.0 kwa mwaka)**.***

Mfuko utafadhili miradi na programu za muda mrefu zinazohitaji muda mrefu kuonyesha matokeo au kukidhi malengo yake. Kama ilivyo kwenye miradi ya vipindi vya kati, Mfuko utatoa kiwango kisichozidi shilingi milioni mia moja (100) kwa mwaka kwa miradi ya muda mrefu.

6.2 Tarehe ya Mwisho ya Kutuma Maombi

Maandiko yote ya miradi yenye kukidhi vigezo yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko kabla ya/au ifikapo tarehe 31 Oktoba 2021. Maandiko ya miradi yatakayotumwa baada ya muda huo hayatafanyiwa kazi na Mfuko katika kipindi husika.

6.3 Mchango wa Mradi kwenye Mipango ya Maendeleo ya Wilaya na Mipango ya Usimamizi ya Misitu lengwa

Miradi ya Maendeleo ya Jamii na ya usimamizi wa maeneo ya hifadhi hufadhiliwa na Mfuko kama sehemu ya Mipango Mikakati ya Wilaya husika na mipango ya usimamizi wa misitu lengwa. Hii ina maana kwamba Maandiko ya Miradi lazima yaendane na vipaumbele vya maendeleo vya Halmashauri za Wilaya lengwa na mipango ya usimamizi ya misitu inayokusudiwa.

6.4 Vipengele Muhimu kwenye Andiko la Mradi

Andiko la Mradi kwa ufadhili wa EAMCEF halipaswi kuzidi kurasa kumi (ukiondoa viambatisho na ukurasa wa juu/nje) na linapaswa kuwa na taarifa za kina katika kila kipengele kifuatacho: -

(i) <u>Muundo wa Maandiko ya Miradi Midogo-Midogo</u>

- Tarehe ya Maombi: _____
- Namba ya Mradi: _____ (itatolewa na EAMCEF)
- Eneo Pendekezwa la Mradi (Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa/Mikoa): _____
- Msitu Lengwa: _____
- Maelezo ya Mwombaji:
  - (i) Jina na Anwani: _____
  - (ii) Hadhi ya Kisheria: _____
  - (iii) Mwaka wa Kuanzishwa: _____

6. Jina, sifa na cheo cha mhusika mkuu (kama ni utafiti weka pia na jina la msimamizi/mshauri mkuu): _____
7. Jina la Andiko la Mradi: _____
8. Aina Kuu ya Andiko la Mradi:_____
9. Malengo ya Mradi na Vipimo vya Utekelezaji: _____
10. Shughuli zilizopangwa (pamoja na malengo halisi na yanayopimika): _____
11. Umuhimu wa Andiko la Mradi pendekezwa (onesha namna mradi wako utakavyosaidia kuchangia katika uhifadhi wa eneo la msitu lengwa): _____
12. Wanufaika wa Mradi: _____
13. Maelezo mafupi ya matokeo tarajiwa ya Mradi: _____
14. Hali Halisi ya Shughuli Inayopendekezwa (kwa mfano: je, kazi ilishaanza, shughuli inayopendekezwa inaendelea? au je, ni mwendelezo wa kazi ya nyuma?): _____
15. Utatekelezaje shughuli inayopendekezwa? _____
16. Muda, Kipindi na Mpango /Ratiba ya Utekelezaji: _____
17. Jumla ya Bajeti ya Mradi (ikionyesha mchanganuo wa kila kipengele) na ikihusisha mchango wa kihisani/hali na kiwango chake:

Shughuli/vipengele vya kazi	Kiasi/kiwango kinachohitajika	Gharama kwa Kiasi/Kiwango (Sh.)	Jumla ya gharama (Sh.)
1.			
2.			
3.			
4.			
5.			
6.			
7.			
8.			
9.			
	Jumla Kuu		
	Kiasi cha fedha kinachoombwa kutoka EAMCEF		
	Kiasi Kitakachotolewa na Wadau wengine		
	Mchango wa hali/mali kutoka kwa Mwombaji		

Onyesha vyanzo vya fedha zitakazotolewa na Wadau wengine: _____

18. Maoni na mapendekezo ya Ofisa Mtendaji wa Kata/Maofisa Watendaji wa Kata:

Jina: _____ Mhuri wa Ofisi: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

19. Maoni na mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya:

Jina: _____ Mhuri wa Ofisi: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

20. Maoni na Mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi inayohusika na Eneo/Msitu Lengwa:

Jina: _____ Cheo: _____ Mhuri wa Ofisi: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

21. Maoni na Mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi inayoomba Ufadhili:

Jina: _____ Cheo: _____ Muhuri wa Ofisi: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

(ii) Muundo wa Maandiko ya Miradi ya Kati /Vipindi Maalumu na ya Muda Mrefu

1. Muhtasari

<table>
<tr><td colspan="2">Jina la Mradi:
Namba ya Mradi: (Itatolewa na EAMCEF)</td><td>Tarehe:</td></tr>
<tr><td>Jina la Mwombaji/Taasisi Inayoomba:</td><td rowspan="3">Jina, Sifa na Cheo cha Mhusika Mkuu/Wahusika Wakuu na Anwani:</td><td>Simu:</td></tr>
<tr><td></td><td>Tovuti:</td></tr>
<tr><td></td><td>Baruapepe:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Hadhi ya Kisheria/Aina ya Taasisi:</td><td>Mwaka Taasisi Ilipoanzishwa:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Eneo la Mradi: Msitu lengwa, Mkoa/Mikoa, Wilaya, Kata, Vijiji, n.k.</td><td rowspan="3">Namna ya Utekelezaji wa Mradi na Taarifa Kuhusu Washirika (kama wapo):</td></tr>
<tr><td colspan="2">Aina kuu ya Mradi Unaoombwa (Maendeleo ya Jamii/Utafiti):</td></tr>
<tr><td colspan="2">Aina ya Ufadhili wa Mradi: (Mradi Mdogo/Kati/Muda Mrefu):</td></tr>
<tr><td colspan="2" rowspan="2">Orodhesha Madhumuni na Malengo ya Mradi/Utafiti na Matokeo Yanayotarajiwa (yasizidi maneno 100):
• Dhumuni:
• Malengo:
• Matokeo Yanayotarajiwa:</td><td>Idadi ya Wanufaika wa Mradi kwa Aina na Kijinsia:</td></tr>
<tr><td>Hali ya Mradi: Andiko Jipya/Andiko Lililoboreshwa Linalowasilishwa Tena/Mradi Unaoendelea:</td></tr>
<tr><td colspan="2">Shughuli Zilizopangwa na Malengo Yanayopimika:</td><td>Namba ya Mradi na Tarehe ya Kuidhinishwa (kwa Mradi Unaoendelea):</td></tr>
<tr><td colspan="2">Matokeo Yanayotarajiwa:</td><td>Sababu kuu za Kuendelea na Mradi (kwa mradi unaoendelea):</td></tr>
<tr><td>Jumla ya Gharama za Mradi (Sh.):</td><td>Jumla ya kiasi kinachoombwa kutoka EAMCEF (Sh.):</td><td>Orodhesha Michango Mingine Ikiwemo ya Hali (Sh.):</td></tr>
<tr><td>Muda wa Mradi kwa Miezi na Muda wa Kuanza hadi Kumalizika kwa Mradi:</td><td>Kiwango Kinachoombwa Kutoka EAMCEF kwa Mwaka wa Fedha Ujao (_____): Sh.</td><td>Eleza Umuhimu wa Mradi ukiainisha sababu za Msingi za kufadhiliwa:</td></tr>
</table>

2. Mapendekezo ya Taasisi Husika

(a) Maoni na mapendekezo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii/Taasisi nyinginezo zinazohusika na Eneo la Msitu Lengwa (Hii ni kwa miradi ya Uhifadhi wa Bioanuwai na Maendeleo ya Jamii tu)

i. Mtendaji Mkuu/ Meneja wa Kanda, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania/Taasisi nyingine Inayohusika (zibainishe)

Maoni /Mapendekezo:

Jina: _____ Mhuri wa Ofisi: _____

Cheo: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

(b) Maoni na mapendekezo kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa na Serikali za Mitaa kwenye Maeneo ya Msitu Lengwa (Hii ni kwa Miradi ya Uhifadhi wa Bioanuwai na Maendeleo ya Jamii tu)

(i) Maoni na Mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya:

_____

Jina: _____Mhuri wa Ofisi: _____

Cheo: _____

Saini:_____ Tarehe: _____

(ii) Maoni na Mapendekezo ya Katibu Tawala wa Mkoa:

_____

Jina: _____ Mhuri wa Ofisi:_____

Cheo: _____

Saini:_____Tarehe:_____

(c) Mapendekezo na Maoni ya Mkuu wa Taasisi Inayoomba (Hii ni kwa miradi ya Utafiti tu):

_____

_____

Jina:_____ Mhuri wa Ofisi:_____

Cheo: _____

Saini: _____ Tarehe: _____

MAELEZO YA KINA

I. Muhtasari wa Mradi

Andiko ni lazima liwe na muhtasari wa kazi inayopendekezwa na libainishe mambo ya msingi yatakayotekelezwa pamoja na matokeo ya utekelezaji huo. Muhtasari huo usizidi ukurasa mmoja na usiwe ufupisho wa andiko bali uwe na maelezo yanayojitosheleza yakionyesha matokeo yatakayopatikana endapo andiko litafadhiliwa. Muhtasari huo unapaswa kuonyesha kwa kina sifa mbili muhimu: (1) Sifa za kitaaluma kuhusiana na shughuli iliyopendekezwa; na (2) matokeo chanya yatakayotokana na shughuli iliyopendekezwa yakionyesha mchango wa mradi kwenye uhifadhi wa misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Muhtasari huo unapaswa kujitosheleza, kueleweka na kuelimisha wadau wengine kwenye fani husika.

Andiko litakalokosa sifa muhimu zilizoainishwa hapo juu halitafadhiliwa.

II. Dhumuni la Mradi

Kwenye kipengele hiki mwombaji anapaswa kueleza kinagaubaga madhumuni ya mradi na mchango wake kwenye malengo makuu ya uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki. Mwombaji ni lazima aonyeshe kwa kina umuhimu wa mradi na sababu za msingi za kupata ufadhili kutoka EAMCEF. Ni lazima andiko lionyeshe kwa kina matokeo ya mradi huo likizingatia mambo ya msingi yafuatayo.; (i) Mchango wa mradi kwenye uhifadhi endelevu wa bioanuwai ya Milima ya Tao la Mashariki kwa kutumia mbinu na ujuzi unaotokana na utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kuongeza na kueneza uelewa kwa kuwajengea uwezo zaidi wakufunzi ; (ii) Mchango wa mradi katika kupanua wigo wa ushiriki wa makundi mbalimbali yasiyo na uwakilishi mzuri (kwa mfano, kijinsia, fursa, maeneo yaliyosahaulika, n.k.); (iii) Mchango wa mradi kwenye uhifadhi wa bioanuwai, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uboreshaji wa hali ya maisha ya jamii, utafiti, elimu na ushiriki kwenye miradi ya maendeleo.; (iv) ni kwa kiasi gani matokeo ya mradi yatasambazwa ili kuchochea uelewa na uhifadhi wa bioanuwai; (v) Faida kwa jamii zitakazotokana na mradi husika; (vi) Mchango wa mradi katika kubadilisha tabia za jamii kuelekea kwenye mtazamo chanya kwa uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki.

III. Malengo-Mkakati na Upimaji wa Utekelezaji

Orodhesha na fafanua malengo mahususi ya mradi. Chini ya kila lengo, onesha uhusiano wa kiashiria cha mafanikio ambacho utakitumia kupima mafanikio ya mradi.

IV. Mbinu za Utekelezaji wa Mradi

Onyesha mikakati utakayotumia kufikia malengo. Sehemu hii inampa mwombaji nafasi ya kueleza mikakati ya utekelezaji itakayomwezesha kufanikisha mradi kufikia matokeo yenye tija. Katika hatua hii, mwombaji anatakiwa aonyeshe mpangilio wa kazi na kila kazi iwe na malengo yanayopimika, kufikiwa kwa urahisi na matokeo yatakayopatikana na kuonesha muda wa kukamilisha kazi za mradi. Kwa miradi ya utafiti, mwombaji anatakiwa kueleza mpango mzima wa utafiti wake.

Sehemu hii lazima itoe maelezo kamili kuhusu kazi itakayofanyika kwenye vipengele vifuatavyo; (a) muda utakaotumika kufanya kazi zilizopendekezwa na faida zinazotarajiwa; (b) uhusiano wa mradi ulioombwa na malengo ya muda mrefu; (c) Uhusiano wa ujuzi/maarifa katika eneo la utekelezaji mradi na shughuli nyingine zinazoendelea zenye kuhusiana na mradi unaopendekezwa. Katika sehemu hii mwombaji anapaswa kuainisha mpango kazi wake, ikiwa ni pamoja na kazi zitakazofanyika, mbinu/njia za utekelezaji pamoja na uhusiano kati ya shughuli za mradi, uhifadhi wa bioanuwai na maendeleo ya jamii, uandaaji taarifa, na ubadilishanaji takwimu/taarifa/uzoefu na wadau wengine wa Milima ya Tao la Mashariki ikiwa ni pamoja na taasisi za utafiti na elimu.

V. Mambo ya Msingi kufanikisha Mradi

Mwombaji atatumia sehemu hii kuchambua na kuelezea mambo muhimu na ya msingi yatakayopelekea kufanikiwa kwa mradi husika ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuhakikisha kuwa mambo hayo yanatekelezwa na kusimamiwa kikamilifu.

VI. Maelezo juu ya Wanufaika

Sehemu hii itatambulisha wanufaika wa mradi na uchambuzi wa kina juu ya ushiriki wao kwenye uandaaji wa mradi husika. Pamoja na hayo andiko ni lazima lionyeshe mikakati mahsusi ya ushirikishaji taasisi mbalimbali zinazohusiana na utekelezaji wa mradi katika eneo husika.

VII. Mpango wa Uperembaji na Tathimini

Katika sehemu hii, mwombaji ataelezea mpango mzima wa uperembaji/ufuatiliaji wa mradi ikiwa ni pamoja na mifumo na mbinu mbalimbali za ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu zitakazotumika kupima maendeleo ya mradi katika kuyafikia malengo yaliyowekwa. Mwombaji anapaswa kuonyesha jedwali la mpango wa upimaji matokeo likionyesha viashiria vyote muhimu pamoja na muda wa ukusanyaji wa taarifa. Mwombaji aonyeshe pia taarifa za awali kuhusu hali ilivyo wakati wa kuanza mradi na mikakati ya uboreshaji.

VIII. Mpango Endelevu

Mwombaji anapaswa kuonyesha jinsi uwekezaji wa EAMCEF kupitia andiko lake utakavyochangia katika uhifadhi endelevu wa Milima ya Tao la Mashariki hususan katika eneo lengwa. Mwombaji ni lazima aeleze jinsi utekelezaji wa mradi husika utakavyochangia katika malengo mapana ya uhifadhi ikiwa ni pamoja na upatikanaji fedha wa uhakika wa kuendeleza matokeo ya mradi husika.

IX. Bajeti

Mwombaji ni lazima aainishe vipengele vya bajeti kwa kila mwaka anaoomba ufadhili. Taarifa kuhusu gharama halisi za utekelezaji wa mradi zitaonyeshwa kwenye sehemu hii ya bajeti. Bajeti ihusishe kiwango cha fedha kinachoombwa kutoka EAMCEF, kiasi kitakachopatikana kutoka kwenye vyanzo vingine na kiasi pamoja na mchango wa mwombaji kwenye mradi husika. Andiko linapashwa pia kuonyesha mapato yatakayotokana na matokeo ya mradi kama yatakuwepo.

Maelezo ya kina yasiyozidi kurasa tano kuhusu ufafanuzi wa gharama mbalimbali za mradi yatatolewa kama kiambatisho. Vipengele vya bajeti lazima viendane na mfumo wa uwasilishaji mahesabu wa EAMCEF unaotumika katika kukusanya na kutoa taarifa za matumizi.

Vipengele vya Bajeti vinavyoweza kugharamiwa na EAMCEF

Vipengele vya bajeti vifuatavyo huidhinishwa na kufadhiliwa na EAMCEF.

a) Mishahara na Posho

Sera

Kwa kawaida, mishahara ya wafanyakazi wa Halmashauri za Wilaya, wafanyakazi wa maeneo yaliyohifadhiwa, wahadhiri wa vyuo na watendaji wengine wanaojishughulisha na miradi inayofadhiliwa na EAMCEF hujumuishwa kwenye bajeti za mwaka za Taasisi husika. Kwa mantiki hiyo, EAMCEF hugharimia shughuli za msingi za utekelezaji wa miradi husika ikiwa ni pamoja na vitendea kazi. Katika hali ya kawaida ufadhili wa EAMCEF ni kwa ajili ya kuchangia shughuli za Taasisi husika na siyo mbadala wa majukumu ya Taasisi. Hata hivyo, EAMCEF kupitia miradi husika hulipa posho ya kujikimu kwa watekelezaji wa miradi pale wanapokuwa wakitekeleza miradi husika nje ya vituo vyao vya kazi. Fedha za ufadhili wa mradi haziwezi kutumika kuongeza mishahara ya wafanyakazi wa Taasisi zinazotekeleza miradi husika.

Mara chache, EAMCEF inaweza kulipa mishahara au honoraria kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi katika mfumo wa ada au fidia ya ushauri wa kitaalamu. Wakati mwingine Taasisi za Utafiti/Elimu ya Juu zinaweza kuajiri wataalamu wa muda mfupi kwa ajili ya shughuli maalumu ndani ya mradi husika na hivyo kulazimika kuwalipa kwa fedha za mradi chini ya ufadhili wa EAMCEF. Hata hivyo, gharama za washauri/wataalamu na wafanyakazi wa muda maalumu hujumuishwa kwenye bajeti kuu ya mradi husika.

Mara nyingi mishahara ya wafanyakazi wa utawala na wahudumu kwenye Taasisi za Elimu ya Juu hujumuishwa kwenye bajeti zao kama sehemu ya gharama isiyokuwa ya moja kwa moja. Hata hivyo, mishahara ya wafanyakazi wa utawala na wahudumu wengine inaweza ikaombwa kama gharama ya moja kwa moja ikiwa mradi unaofadhiliwa na EAMCEF unahitaji kiwango kikubwa cha usaidizi wa wafanyakazi wa utawala na wahudumu. Mazingira yanayosababisha uhitaji wa gharama hizo kwenye mradi husika yanapaswa kufanyiwa upembuzi na kuhakikisha kuwa gharama hizo zinakuwa wazi na sahihi kikamilifu.

EAMCEF haitawajibika kwa namna yoyote na mkataba wowote wa ajira ambao Mnufaika wa Mradi ameingia na mtu yeyote au taasisi, katika kipindi cha utekelezaji wa mradi unaofadhiliwa na EAMCEF.

(b) Taratibu za Kufadhili Tafiti

Maandiko ya miradi ya utafiti yanapaswa kuonyesha orodha ya Watafiti Wakuu/Viongozi, wataalamu mbalimbali watakaoshiriki kwenye mradi pamoja na makadirio ya muda utakaohitajika kwenye mradi lengwa na malipo/mishahara yao kwenye mwaka wa masomo husika (kwa miradi ya utafiti kwenye Vyuo Vikuu).

Orodha ya wataalam/watafiti wenye elimu ya Udaktari wa Filosofia na kuendelea pamoja na Watafiti Waandamizi na wataalamu wengine ijumuishwe kwenye andiko ikionyesha idadi ya wahusika katika kila sekta ya Mradi husika, miezi atakayoshiriki kwenye utafiti na kiwango cha mshahara wake kwa mwaka. Maelezo yatolewe pia kuhusu wahitimu na wanafunzi wa shahada ya kwanza, makatibu muhtasi, makarani na wasaidizi wengine, watakaoshiriki kwenye mradi ambao muda wao utalipwa moja kwa moja kupitia mradi husika. Ni vyema pia kutoa taarifa kuhusu idadi yao na kiasi cha mishahara kinachohitajika kwa mwaka husika ndani ya kipindi cha mradi. Maombi ya mishahara kwa ajili ya miradi ni lazima yaendane na utaratibu wa kawaida wa malipo wa Taasisi husika na yakidhi taratibu za EAMCEF za fedha. Uchambuzi wa bajeti unapaswa kuonyesha kwa undani taarifa za kiwango cha malipo kwa kila mhusika katika ngazi zote. Mradi unaweza pia kuomba fedha kwa ajili ya watafiti wasaidizi (wanafunzi) iwapo watahitajika kusaidia shughuli za utafiti kama itakavyoonekana inafaa. Malipo yote yanayohusiana na mishahara yatapaswa kujumuishwa kwenye kipengele cha Mishahara na Posho/masurufu kwenye andiko la mradi.

(c) Manunuzi ya Vifaa

Kwa mujibu wa sera za EAMCEF, kifaa maana yake ni kitu chenye thamani ya Sh. 50,000/= au zaidi na chenye kudumu kwa muda wa mwaka mmoja au zaidi. Vifaa vyote vya mradi vitaorodheshwa kwenye andiko vikionyesha aina, uhitaji na thamani ya kila kifaa. Vifaa vitakavyoidhinishwa na EAMCEF ni vile vyenye umuhimu kwenye utekelezaji wa mradi ambavyo havipatikani kwenye Taasisi husika kwa wakati huo. EAMCEF haitaidhinisha ununuzi wa vifaa kama vile kompyuta mpakato ila inaweza kulipia gharama za uchambuzi wa takwimu, maabara, nk kupitia Taasisi mbalimbali za Elimu na Utafiti zinazojishughulisha na kazi hizo. Vifaa vyote vilivyonunuliwa kupitia fedha za ufadhili wa miradi ya EAMCEF vitabaki kuwa mali ya EAMCEF na vitaorodheshwa kwenye leja za EAMCEF hadi mradi husika utakapomalizika ambapo EAMCEF itaamua njia sahihi ya kuvitoa kwa wadau au kuvitumia kama itakavyoonekana inafaa. EAMCEF inaweza pia kununua vifaa vya mradi kwa niaba ya mnufaika badala ya kumpatia fedha za vifaa husika kulingana na thamani na aina ya kifaa kama itakavyoonekana inafaa.

(d) Vitendea kazi, Nyenzo na Mahitaji mengine ya Mradi

EAMCEF huidhinisha fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi, nyenzo na mahitaji mbalimbali ya utekelezaji wa mradi. Malipo yote ya ununuzi wa vitendea kazi au huduma ni lazima yazingatie taratibu sahihi za manunuzi ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa bei ya bidhaa/huduma kutoka kwa watoa huduma watatu au taratibu nyinginezo za manunuzi ya umma zinazokubalika. Malipo ya baadhi ya huduma/kitendea kazi/bidhaa nk yanaweza kulipwa moja kwa moja na EAMCEF kurahisisha utekelezaji wa mradi ikionekana ina tija zaidi.

(e) Usafiri

(i) Utangulizi

Usafiri ndani ya Tanzania unaohusiana na utekelezaji wa mradi ni lazima uainishwe kwa kila kipengele ukionyesha sehemu anayokwenda mhusika na gharama halisi. Fedha za usafiri zinaweza kuombwa kwa ajili ya utendaji kazi maeneo ya mradi, kuhudhuria mikutano na warsha na safari nyingine zinazohusiana na mradi husika ikiwa ni pamoja na posho za kujikimu. Hata hivyo, EAMCEF itafadhili safari za kuhudhuria mikutano na warsha mbalimbali ikiwa vitaongeza uwezo wa mwombaji wa utekelezaji mradi, upanuaji au usambazaji wa matokeo ya mradi. Katika hali ya kawaida EAMCEF haitagharamia usafiri wa anga.

(ii) Usafiri wa nje ya nchi

Katika mazingira machache sana na ya kipekee, EAMCEF inaweza kugharamia safari za nje.

Pendekezo lolote la safari ya nje ni lazima liwe na taarifa zinazojitosheleza ikiwa ni pamoja na nchi zitakazotembelewa, tarehe za safari kama zinajulikana na sababu za kina za safari hizo katika mradi lengwa. Mwombaji atapaswa kuwasilisha kwa EAMCEF hoja nzito na yenye mashiko kuhusu sababu na ulazima wa kusafiri nje ya nchi kwa ajili ya mradi lengwa. Mara nyingi EAMCEF haifadhili safari za nje ya nchi.

(f) Ufadhili wa Gharama za Ushiriki Kwenye Matukio Mbalimbali

Hii inahusu gharama za usafiri, posho za kujikimu, na gharama nyinginezo zinazohusiana na ushiriki kwenye mafunzo au makongamano mbalimbali yenye tija kwenye shughuli za EAMCEF. Idadi ya washiriki na gharama zao itajumuishwa kwenye bajeti ya mradi na mchanganuo wake ni lazima uonyeshwe kwenye uchambuzi wa bajeti.

(g) Gharama nyinginezo

Gharama zote zinazohusiana na miradi inayofadhiliwa na EAMCEF ni lazima zijikite kwenye shughuli iliyokubaliwa na kuidhinishwa. Bajeti ya mradi ni lazima ionyeshe na kuainisha gharama nyinginezo zinazohusiana na mradi ambazo hazipo katika vipengele vilivyoainishwa hapo juu, ikiwa ni pamoja na vifaa na usambazaji wake, gharama za uchapishaji, huduma za kompyuta na huduma za ushauri wa kitaalam. Mifano ya gharama hizi ni kama kukodi ndege, kukodi eneo au nyumba pale ambapo ni mbali kutoka kwenye taasisi inayofadhiliwa, matengenezo madogo ya nyumba, malipo ya watu, gharama za huduma na utengenezaji wa vifaa au mifumo ambayo haipo. Vitabu vya rejea na majarida yanayotolewa kwa kipindi maalumu yanaweza kulipiwa na mradi ikiwa tu yanahitajika kwa ajili ya mradi husika.

(h) Ada kwa ajili ya Mawakala, Asasi na Taasisi za Utafiti

Viwango vya ada mbalimbali kwa ajili ya Wakala, Asasi, Taasisi za Utafiti nk zitajadiliwa kati ya EAMCEF na Mnufaika pale ambapo kiwango kinazidi asilimia 20% ya bajeti inayopendekezwa kwa ajili ya mradi mzima.

(i) Uchangiaji wa Gharama

Ufadhili wa EAMCEF unawataka wanufaika wake kuchangia gharama za mradi. Maandiko yanayotumwa EAMCEF lazima yaonyeshe mchango wa mwombaji kwenye mradi husika. Kwenye baadhi ya mazingira uchangiaji unaweza kuwa wa hali. Wakati wa kuthaminisha mchango wa hali mwombaji anaweza kutumia viwango vya gharama za posho zinazotumika katika eneo la mradi, mishahara ya watumishi pamoja na vifaa mbalimbali vya taasisi kama ofisi, vyombo vya usafiri, kompyuta nk katika kukadiria mchango wa hali kwenye mradi husika.

X. Viambatisho

Iwapo kuna taarifa za ziada zinazohusiana na mradi zitatolewa kama viambatisho. Kiambatisho cha kwanza kitakuwa mchanganuo na maelezo ya kina kuhusu bajeti. Viambatisho vingine vinaweza kuhusisha taarifa rasmi au za ziada ili kuboresha maombi ya ufadhili. Taarifa hizo zinaweza kujumuisha ramani, utafiti uliokwishafanyika na kukamilika, barua za maoni kutoka kwa Washirika/Wadau wa EAMCEF, taarifa za tathmini za athari za kimazingira na taarifa nyinginezo muhimu zinazohusiana na mradi husika.

Taarifa ya ziada inaweza pia kujumuisha taarifa kwa EAMCEF kuhusu mazingira yasiyokuwa ya kawaida yanayohitaji kushughulikiwa kwa umakini kama vile mambo yanayoweza kuingilia haki miliki, faragha, usalama wa taifa, nk.

Kwa maandiko yote ya utafiti, taarifa za marejeo zitatolewa kama kiambatisho. Kila rejeo ni lazima lijumuishe majina ya waandishi wote (kwa mfuatano uleule uliopo kwenye chapisho), jina la makala au jarida, jina la kitabu, namba ya juzuu/toleo, namba ya kurasa na mwaka wa kuchapishwa. Kama chapisho linapatikana kwa njia ya kielektroniki, anwani ya tovuti ionyeshwe pia. Waombaji lazima wawe makini zaidi katika kufuata utaratibu wa kitaaluma wa kuonyesha dondoo za marejeo kwa vyanzo vya machapisho waliyoyatumia wakati wa uandaaji wa sehemu yoyote ya aandiko la mradi. Pamoja na kuwa hakuna kiwango cha idadi ya marejeo sehemu hii lazima pia ihusishe dondoo za bibliografia.

7. Namna ya Kuomba

Maandiko kamilifu yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko kwa nakala tepe (soft copies) na nakala ngumu (hard copies) kwa anuani iliyotolewa hapo chini kabla ya tarehe ya mwisho ya kutuma

maombi. Maombi yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya mkono, posta au baruapepe. Maombi yaliyotumwa kwa njia ya baruapepe yafuatiwe na utumaji wa nakala ngumu halisi zilizosainiwa kwa ukamilifu ndani ya muda uliotolewa.

Mkurugenzi Mtendaji,
Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki,
Kitalu Na. 348, Eneo la Forest Hill,
Barabara ya Kingalu,
S.L.P 6053,
MOROGORO-Tanzania.

Simu ya Mezani: **+255 23 293 4274**
Simu ya Mkononi: **+255 755 330 558**
Baruapepe: **eamcef@easternarc.or.tz**
Tovuti: **www.easternarc.or.tz**

Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi wasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko kwa kutumia anwani iliyowekwa hapo juu.

NYOTE MNAKARIBISHWA